...ndoa migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji

# DC Kiteto awapa somo wakulima, wafugaji kuhusu utunzaji ardhi

**NA LILIAN JOEL,** KITETO

MKUU wa Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Tumaini Magesa, amewataka wafugaji na wakulima katika vijiji vya Kimbo, Allole na Napalai, vinavyounda ushirika wa "Olengapa" kutunza ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo, kuheshimu utaratibu wa hati miliki za kimila na usajili wa ushirika huo.

Tumaini alitoa rai hiyo jana katika Kijiji cha Eng'ang'ongare, wakati akikabidhi hati miliki za kimila tisa na vyeti, zilizofadhiliwa na Programu ya GSI-ICCA kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na kusaidiwa na Umoja wa Ulaya (EU), kupata usajili wa ushirika wao katika vijiji hivyo.

Alisema lengo la UNDP na EU kuwasaidia wafugaji hao kwa ajili ya kuendeleza nyanda za malisho, zilizopo katika mpango wa kimataifa wa kuendeleza maeneo yaliyohifadhiwa kwa kutumia taratibu za kiasili au kimila na kutekelezwa na Jumuiko la Mali Asili Tanzania (TNRF) na Muungano wa Vijiji vya Wafugaji kwa Ajili ya Kusaidiana (KINNAPA).

Magesa alisema ni vizuri kila eneo matumizi yake yawe yamepangwa na kujulikana kisheria, ili kuondoa changamoto ya migogoro ya ardhi, iliyokuwa ikijitokeza wilayani humo, miaka iliyopita.

"Tunapotunza ardhi hizi tunaondokana na migogoro isiyo ya lazima, lakini tunahifadhia vizazi vijavyo na vya sasa," alisema.

Kwa upande wake mmoja wa wananchi hao kutoka kijiji cha Kimbo akizungumza kwa niaba ya wenzake, Rehema Barhe, alisema wao kama wanawake wa jamii ya kifugaji na wananchi wengine, wamefurahia mpango huo ambao utakuwa chachu kubwa ya kupiga hatua ya maendeleo na kumaliza changamoto ya migogoro ya ardhi iliyokuwa ikijitokeza baina ya wafugaji na wakulima.

Mkurugenzi wa Jumuiko la Mali Asili Tanzania (TNRF), Zacharia Fustin, alisema hatua ya serikali kuruhusu sera na sheria zitumike kutatua migogoro ya ardhi, pamoja na kukabidhi hati miliki za Kimila kwa jamii ya kifugaji, kutamaliza migogoro ya rasilimali ardhi kwa wakulima na wafugaji.

Mratibu wa KINNAPA, Abrahamu Akilimali alisema lengo la mpango huo kuhakikisha maeneo yaliyohifadhiwa kiasili yawe na umiliki wa kisheria ili kutunza na kulinda rasilimali ardhi na asili, pamoja na kumaliza migogoro ya ardhi.

Hati miliki za kimila tisa na vyeti vitatu vya usajili wa ushirika wa wafugaji wa kuendeleza nyanda za malisho, vilivyotolewa kwa vijiji vitatu, vimehusisha ukubwa wa eneo la ardhi kilomita za mraba 7,348.

'FASHIONS'

Scanned with CamScanner

AFYA

# Mtaalamu Mifugo anyambua viboko, mizigo, kuwafungia kunavyowatesa

## •Unajua adhabu sheria kumchapa mnyama?

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

[illegible]



Punda wakibebeshwa mizigo kupita kiasi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### MTAALAMU MIFUGO

[illegible]

### HAKI ZA WANYAMA

[illegible]

### MAONI YA WAFUGAJI

[illegible]

### WATETEZI WANYAMA

[illegible]

### MENEJA PROGRAMU

[illegible]

### CHAMA CHA WAFUGAJI

[illegible]



Mchungaji wilayani Babati, akiwapeleka ng'ombe malishoni. **PICHA: JALIWASON JASSON**

Scanned with CamScanner



**NAONJA: Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (kulia), akionja kipande cha kiazi lishe alipotembelea kiwanda cha kusindika unga wa viazi lishe kilichopo mkoani Simiyu juzi.**

SIMIYU

# Nanenane kitaifa kufanyika Simiyu

**Na MWANDISHI WETU**

MAADHIMISHO ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) kitaifa yatafanyika Viwanja vya Nyakabindi, Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu kuanzia Agosti Mosi.

Akizungumza na waandishi wa habari akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Songwe, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema maonyesho hayo yataambatana na uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia bora za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Alisema yatashirikisha wadau mbalimbali zikiwemo wizara, taasisi za umma na binafsi, wabia wa maendeleo, wakulima na vyama vya wakulima, wafugaji na wavuvi.

Hasunga alisema pia maonyesho hayo ya 28 yatafanyika kwenye kanda nane ambazo ni Mashariki (Morogoro), Kaskazini (Arusha), Magharibi (Tabora), Kusini (Lindi), Kati (Dodoma), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Ziwa Mashariki (Simiyu) na Ziwa Magharibi (Mwanza).

Alisema lengo la maonyesho ya Nanenane katika kanda hizo ni kutoa fursa kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wanaushirika kuona na kujifunza matumizi ya teknolojia bora za kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuongeza tija na uzalishaji wa chakula, kukidhi mahitaji ya viwanda na masoko ya ndani na nje ya nchi.

Kaulimbiu ya maonyesho ya mwaka huu inasema 'Kwa Maendeleo ya kilimo, mifugo na uvuvi chagua viongozi bora 2020'.

"Mwaka 2020 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu, hivyo kaulimbiu hii inatoa hamasa kwa wananchi kuchagua viongozi bora watakaokuwa chachu ya kuleta mapinduzi kwa ajili ya maendeleo ya sekta za kilimo ili kuinua ustawi wa maisha ya wakulima, wafugaji na wavuvi," alisema Hasunga.

MWANZA

# Wanaume washauriwa kuongozana na wenzi wao kuhudhuria kliniki

UHURU

MAONI YA MHARIRI

# Machinjio mapya ya Vingunguti kuongeza ubora wa nyama nchini

HIVI karibuni Baraza la Wazee la Mkoa wa Dar es Salaam lilielezea kuridhishwa na ujenzi wa machinjio ya mapya ya Vingunguti, huku vifaa vya kisasa vikitarajiwa kuwasili nchini Julai 15, mwaka huu.

Hayo yalijiri wakati wa ziara ya viongozi na wajumbe wa baraza hilo ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa machinjio hiyo, ambapo walimpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katibu wa Baraza hilo, Mohammed Mtulia, alisema dhamira ya ziara yao ilikuwa ni kujionea utekelezaji wa Ilani katika mradi huo wa kimkakati ambao utakuwa chachu kubwa katika kuinua uchumi na kuongeza ajira.

Mjumbe wa Baraza hilo na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Wilaya ya Temeke, Mohammed Bonde, alisema kukamilika kwa machinjio hayo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Diwani mstaafu wa Kata ya Vingunguti, Omari Kumbilamoto, alisema mradi uko katika hatua za mwisho kukamilika na utaleta ajira nyingi hususan watu zaidi ya 300.

Haya ni mafanikio makubwa kwa kuwa sasa wananchi hususan wa mkoa wa Dar es Salaam, watapata huduma bora na za kisasa katika kujipatia nyama iliyoandaliwa katika mazingira mazuri.

Mradi huo ambao unagharimu zaidi ya sh.bilioni 12 zilizotolewa na serikali na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, utarahisisha shughuli za uchinjaji wa mifugo na hivyo kuweza kufikishwa sokoni kwa wakati.

Tunasema hivyo kwa sababu machinjio hayo yatafungwa vifaa vya kisasa kwa ajili ya maandalizi, uchinjaji na kupelekwa sokoni ikiwa salama na katika ubora unaohitajika.

Lakini lililo bora zaidi ni kwamba machinjio hayo yataongeza kasi ya uandaaji nyama tofauti na ya sasa ambayo uwezo wake ni mdogo, licha ya kulalamikiwa kuwa na mazingira duni.

Pia yatatoa fursa ya ajira kwa watu wasiopungua 300 na hivyo kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hususan kwa vijana ambao wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa ajira za moja kwa moja.

Tunaamini kupitia machinjio hayo, maduka makubwa ya bidhaa katika Jiji la Dar es Salaam, sasa yatapata nyama ya uhakika na kwa kiwango kinachohitajika ili kukidhi mahitaji ya soko la bidhaa hiyo.

Ni matarajio yetu mradi huo utakamilika katika muda uliopangwa na shughuli za uchakataji wa nyama kuanza na hivyo kuongeza wigo wa mapato ya serikali na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kwa ujumla.

Uhuru Media Group (UMG)
S.L.P. 9221, Dar es Salaam.

Scanned with CamScanner